

## HALMASHAURI YA WILAYA YA BAHI

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri)

Simu: +255 26 2961400  
Nukushi.: +255 26 2961401  
Barua pepe: [info@bahidc.go.tz](mailto:info@bahidc.go.tz)  
[ded@bahidc.go.tz](mailto:ded@bahidc.go.tz)  
Tovuti: [www.bahidc.go.tz](http://www.bahidc.go.tz)



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,  
S. L. P. 2993,  
DODOMA,  
TANZANIA.

### TAARIFA KWA UMMA

MKUU WA WILAYA YA BAHI, MHE. ELIZABETH S. KITUNDU ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE WILAYANI BAHI KUWA KUENZIA TAREHE 16/10/2017 HADI TAREHE 22/10/2017 KUTAKUWA NA HUDUMA YA MADAKTARI BINGWA KATIKA KITUO CHA AFYA MUNDEMU, MADAKTARI BINGWA HAO WATATOA HUDUMA YA MAGONJWA MBALIMBALI KAMA IFUATAVYO:-

#### DAKTARI BINGWA WA WATOTO:

- ATATOA HUDUMA KWA MAGONJWA YOTE YA WATOTO, IKIWA NI PAMOJA NA WENYE MIDOMO WAZI, VICHWA VIKUBWA, MAGONJWA YA MOYO KWA WATOTO, WATOTO WENYE UVIMBE MWILINI, N.K.

#### DAKTARI BINGWA WA MAGONJWA YA WANAWAKE:

- ATATOA HUDUMA KWA MAGONJWA YOTE YA AKINA MAMA, UVIMBE TUMBONI, MATATIZO YA UZAZI NA UJAUZITO, UPIMAJI WA SARATANI YA SHINGO YA KIZAZI, UPASUAJI MDOGO NA MKUBWA, N.K.

#### DAKTARI BINGWA WA KINYWA NA MENO:

- ATATOA HUDUMA KWA MAGONJWA YOTE YA KINYWA NA MENO, KUTOBOKA KWA MENO, UVIMBE MDOMONI, MATATIZO YA FIZI NA ULIMI, UNG'OAJI WA MENO, KUZIBA, UPASUAJI, UTENGENEZAJI WA MENO BANDIA, N.K.

#### DAKTARI BINGWA WA MAGONJWA YA NDANI:

- ATATOA HUDUMA KWA MAGONJWA YA NDANI YOTE, MAGONJWA YAKUAMBUKIZA NA YASIO YA KUAMBUKIZA YOTE, KISUKARI, MAGONJWA YA MOYO YOTE PAMOJA NA SHINIKIZO LA DAMU, MAGONJWA YOTE YA TUMBO, KIFUA, KICHWA, N.K.

#### DAKTARI BINGWA WA MIFUPA:

- ATATOA HUDUMA KWA MAGONJWA YOTE YA MIFUPA NA MISULI, UPASUAJI MDOGO NA MKUBWA, KUUNGA MIFUPA, N.K.

#### DAKTARI BINGWA WA NJIA YA MKOJO:

- ATATOA HUDUMA KWA MAGONJWA YOTE YA NJIA YA MKOJO, IKIWA NI PAMOJA NA KUZIBA KWA MKOJO, TEZI DUME, KUVIMBA KIBOFU CHA MKOJO, MATATIZO YA UZAZI KWA WANAUME, N.K.

**DAKTARI BINGWA WA MACHO:**

- ATATOA HUDUMA KWA MAGONJWA YOTE YA MACHO, KAMA KUTOONA, UVIMBE KWENYE MACHO, PRESHA YA MACHO, MTOTO WA JICHO, UPIMAJI WA MACHO, UPASUAJI NA HUDUMA YA MIWANI. N.K.

**DAKTARI BINGWA WA UPASUAJI:**

- ATATOA HUDUMA YA UPASUAJI KWA WAGONJWA WOTE WENYE UVIMBE MBALIMBALI KWENYE MWILI IKIWA PAMOJA NA UVIMBE KWENYE SHINGO (GOITA), UVIMBE SEHEMU ZA SIRI, NGIRI KAVU(HENIA), NGIRI MAJI (MABUSHA), N.K
- HUDUMA ZA VIPIMO VYOTE VIKUBWA NA MUHIMU VITAPATIKANA, PAMOJA NA ULTRASOUND, ECHO, ECG, X-RAY, NA VIPIMO VINGI VYA MAABARA.

HUDUMA HII ITASAIIDIA WAGONJWA WOTE WALIOHITAJIKA KWENDA HOSPITALI KUBWA ZA KCMC, BUGANDO, MUHIMBILI, DODOMA MJINI NA KUKOSA NAFASI YA KWENDA HUKO KUTOKANA NA UMBALI NA GHARAMA SASA HUDUMA HIZO ZITAPATIKANA TAREHE TAJWA HAPO JUU KWA GHARAMA NAFUU.

KILA MWANANCHI ANAYEHITAJI HUDUMA HII ANATAKIWA KUFHAMU YAFUATAYO:-

- a) HUDUMA HII **SIO BURE**, ITAKUWA NA GHARAMA NAFUU SANA.
- b) KWA WASIO NA KADI YA BIMA YA AFYA YA TAIFA NA CHF WATATOA GHARAMA YA KUMWONA DAKTARI BINGWA **TSH. 5,000/=**, GHARAMA ZA VIPIMO, KITANDA NA DAWA ATALIPIA KULINGANA NA TATIZO ALILONALO, GHARAMA ZA UPASUAJI ITAKUWA **TSH. 30,000/=** TU.
- c) WENYE BIMA ZA AFYA NHIF NA CHF, WATATIBIWA KWA KUTUMIA KADI ZAO ZA BIMA ZILIZO HAI KWA MUJIBU WA MIONGOZO YA MIFUKO HUSIKA, NA YEYOTE ATAKAEJARIBU KUJA NA KADI FEKI HATUA KALI ZITACHUKULIWA DHIDI YAKE.

**Imetolewa na,**

  
Benton Nollo,

**AFISA HABARI (W)**

**BAHI**

**12 OKTOBA 2017**